# Ni Nini Kimekosekana Katika Picha Hii?

**Soma Mwanzo 1:21-28.** Sasa tazama picha. Ni mambo gani yanayokosekana katika picha hii? Andika majibu yako kwenye mistari iliyo hapa chini. Unganisha nukta katika picha, kisha uipake rangi.

**1**. ............................................................

**2**. ............................................................

**ZUNGUMZENI PAMOJA:** Mungu alikuwa akiongea na nani aliposema, "Na tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu"? DOKEZO: Soma Yohana 17:1, 5; Wakolosai 1:15, 16. Ni kwa njia gani wanadamu wameumbwa kwa mfano wa Mungu? DOKEZO: Soma Wakolosai 3:10; 1 Petro 1:16. Ni sifa gani za Yehova Mungu na Yesu zinazokuvutia zaidi? Unaweza kuiga sifa zao jinsi gani? DOKEZO: Soma Waefeso 4:31,32; 1 Yohana 4:7, 8.

**UTENDAJI WA FAMILIA:** Orodhesha wanyama watano unaowapenda zaidi. Kisha, kama Adamu, wape wanyama hao majina mapya kwa kutegemea jinsi wanavyoonekana, sauti wanayotoa, au wanavyotenda. Soma jina hilo kwa sauti na uone ikiwa wengine katika familia watajua huyo ni mnyama yupi.




Ili uchapishe nakala za ziada za "Mazungumzo ya Familia," nenda kwenye **www.jw.org**

**1.** Kiumbe kinachoruka chenye mabawa.
**2.** Mnyama-mwitu.

www.jw.org © 2012 Watch Tower Bible and Tract Society of Pennsylvania